COMPETENCE BASED ASSESSMENTS

GREDI LA TANO

KISWAHILI

MJARABU WA UFUNGUZI WA MUHULA WA 3 2023

SHULE:

……

……

JINA:

……

……

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA.
Swali la 1 hadi la 5.
Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.

(Ni jioni Katana na Mangwana wamekutana dukani)

Katana : (*Akitabasamu)* Hujambo Mangwana? Jambo gani linakuleta hapa wakati huu ilhali mna duka lenu.

Mangwana : *(Akionekana kukasirika*) Sijambo, kwani unaona kuwa mimi sitakiwi kutangamana na marafiki zangu? Acha madharau bwana?

Katana : Samahani ndugu. Sikujua umefika dukani kwa lengo tofauti. Nilidhani umekuja kununua bidhaa.

Mangwana : Ha! Ha! Ha! Najua ni kawaida yako kunifanyia mzaha. Haya basi, ninunulie chipsi.

Katana : *(Kwa furaha)* Hukumbuki kuwa tulishauriwa na mwalimu wetu kutokula vyakula ovyo ovyo? Wajua unaweza kuambukizwa ugonjwa ukatapika na hata kuendesha. Usipotibiwa unaweza kuaga dunia.

Mangwana : Hakika nakubaliana nawe. Juzi rafiki yangu Tina alikula maandazi yaliyokuwa yakichuuzwa barabarani. Alimalizia hospitalini alikopatikana na ugonjwa uitwao waba.

Katana : Kwa hivyo tahadhari kabla ya hatari. *(Wanaagana na kuondoka)*

1. Badala ya Katana kumwamkua Mangwana hujambo? Ni salamu gani nyingine angetumia kumwamkua?

   A. Sabalkheri
   B. Masalkheri
   C. Lala salamu